Akaunti ya Malipo: **10110000587**

# HATI FUNGANI ZA NMB

## Programu ya utoaji wa TZS bilioni 20 kati ya TZS bilioni 200 za muda wa kati

## FOMU YA MAOMBI

(FOMU HII HAIUZWI)

Mwombaji mtarajiwa anapaswa kusoma Memoranda ya Taarifa kabla ya kujaza fomu hii. Nakala ya Memoranda ya Taarifa inaweza kupatikana kwa mawakala wowote wa mauzo walioidhinishwa (ikiwa ni pamoja na Tawi lolote la NMB) ambao walioorodheshwa katika Memoranda ya Taarifa.

Ofa ya kutoa Hati fungani za NMB zenye kiwango cha chini cha TZS 500,000

OFA ITAFUNGULIWA: Tarehe 10 Juni, 2019
OFA ITAFUNGWA : Tarehe 8 Julai, 2019

Tafadhali rejea katika kanuni na masharti yaliyomo katika Memoranda ya Taarifa pamoja na maelekezo ya kujaza Fomu kama yalivyowekwa hapo chini, kabla ya kujaza fomu hii. Masharti yaliyomo humu yatachukuliwa kama yalivyoelezwa katika Memoranda ya Taarifa ya tarehe 3 Mei, 2019.
Bodi ya Wakurgenzi ya National Microfinance Bank Plc ("Wakurugenzi") itakataa maombi yoyote kwa ujumla au kwa sehemu, kama maelekezo yalivyoandikwa katika Memoranda ya Taarifa na Fomu hii ya maombi yatakuwa hayajafuatwa.

### TAMKO LA MUOMBAJI

Kwa kusaini Fomu hii ya Maombi Mimi/ Sisi waombaji tuliomo humu tunakiri kwamba:-

- Ninao/Tunao uwezo kamili wa kisheria wa kuingia mkataba, tumeisoma Memoranda ya Taarifa, hivyo tumeamua kutuma maombi na kukuomba ukubali maombi yangu/yetu kwa kiwango cha fedha kilichotajwa hapo chini, au kiwango chochote cha chini ambacho kinaweza, kwa busara yako, kutolewa kwangu/kwetu kulingana na Kanuni na Masharti ya NMB.
- Mimi/Sisi tunaiidhinisha NMB kuingiza jina langu/majina yetu katika rejista ya wamiliki wa Hati fungani na kuweka kiwango cha Hati fungani ambazo zimegaiwa kwangu /kwetu katika akaunti yangu ya CDS na kurejesha zidio kwangu/kwetu kwa njia ya Uhamishaji wa Fedha Elektroniki au Hundi kulingana na Kanuni na Masharti yaliyomo katika Memoranda ya Taarifa.
- Mimi/Sisi tunaidhinisha Msajili kutuma Fomu yangu/yetu ya Mkopo wa nyumba (mortgage) moja kwa moja kwenda DSE na benki inayotoa mkopo kwaajili ya kununulia Hati fungani.
- Katika kuzingatia kukubali kwako kupokea Fomu hii ya Maombi, Mimi/ Sisi tunakubali kwamba maombi haya hayatatenguliwa na kuandaa mkataba ambao utanilazimu/utatulazimu kupeleka kwa njia ya posta au kufikisha kwa mkono.

### MAELEKEZO YA JUMLA YA KUJAZA FOMU YA MAOMBI

1. Tafadhali jaza fomu hii ya Maombi kwa herufi kubwa ukitumia peni nyeusi/bluu. Hakikisha kila herufi imeandikwa vizuri ndani ya viboksi ulivyopewa. Fomu zitakazojazwa vibaya zitakataliwa.
2. Unapojaza Fomu hii ya Maombi tambua kwamba Hati fungani hazitatumika kwa majina ya wadhamini ambao hawajasajiliwa au waliokufa.
3. Wadhamini wanaotoka katika kampuni ambazo hazijasajiliwa, wabia binafsi au wasimamizi wa mirathi wanaweza kuomba Hati fungani kwa kutumia majina yao. Kampuni zilizosajiliwa zinaweza kuomba kwa kutumia majina ya usajili wa kampuni. Ubia wenye ukomo unaweza kuomba kwa kutumia majina yao ya usajili.
4. Ubadilishaji wowote wa Fomu ya Maombi (zaidi ya ufutaji wa mibadala) lazima uthibitishwe kwa saini za Waombaji au Wakala wa Mauzo aliyeidhinishwa.
5. Wakala wa Mauzo aliyeidhinishwa lazima asaini nakugonga mhuri rasmi wa kampuni.
6. Malipo ya hundi za benki ( Banker's cheque ) lazima yaandikwe au yalipwe kwa "NMB Bond Issue"- ("Fomu ya Malipo Namba xxxx)" na "zisifunguliwe" ( Crossed Account Payee Only )
7. Fomu yako ya Maombi lazima ipokelewe ikiwa imejazwa kikamilifu na kuambatishwa na uthibitisho muhimu wa malipo ya hundi ya benki au Barua ya Ahadi.
8. Fomu ya Maombi iliyojazwa inaweza kutumwa kwa njia ya posta au kwa mkono kwenda kwa Mawakala wa Mauzo na lazima ipokelewe na Wakala wa Mauzo Aliyeidhinishwa sio zaidi ya saa 11 jioni ya tarehe 8 Juni, 2019.
9. Kama Fomu yako ya Maombi itapokelewa na Wakala wa Mauzo Aliyeidhinishwa baada ya saa 11.00 jioni ya tarehe 8 Juni, 2019 itakataliwa. Fomu pamoja na malipo yaliyoambatishwa au uthibitisho wa malipo vitarejeshwa kulingana na kanuni na masharti ya ofa.
11. Maombi yanaweza kuombwa kupitia Wakala wa mauzo aliyeidhinishwa, Waandaaji, Benki itakayopokea na Msajili kama ilivyoorodheshwa katika Memoranda ya Taarifa.
12. Mchakato wa ugawaji umeelezwa katika Memoranda ya Taarifa na Taarifa za nyongeza zinazohusu Bei. Hakuna mtu anayeweza kuahidi kinyume na vigezo vya ugawaji.

Akaunti ya Malipo: **10110000587**

# Fomu ya maombi ya Hati fungani

Andika ndani ya boksi tu

| NZURI | | | MBAYA | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S | T | A | S | T | A |

**HATI FUNGANI YA NMB**
**Fomu ya Maombi ya Ofa kwa Umma**

**TAFADHALI ANDIKA KWA HERUFI KUBWA UKITUMIA PENI NYEUSI/BLUU**

## A. NAMBA YA AKAUNTI YA CDS (LAZIMA) (KAMA HAIPO TAFADHALI JAZA FOMU YA KUFUNGUA CDS AKAUNTI)

Namba ya Akaunti ya CDS (isianze na sifuri)

(LI/LC/FI/FC)

## B. TAARIFA ZA MAOMBI NA MALIPO

Kiwango Kilichoombwa kwa (TZS)

Tafadhali weka alama ya vema (v) panapohusika

**Broker** ☐ **Tawi la NMB** ☐ **NMB Mobile (KLIK)** ☐ **NMB Wakala** ☐ **Mobile Money** (Tigo,Voda,Airtel, etc.) ☐ **Hundi ya Benki** ☐

Namba ya Kumbukumbu

**Benki Nyigine** ☐

Jina la Benki (Lililofupishwa) (kwaajili ya EFT/TISS/Malipo ya Hundi)

Jina la Tawi

## C. IKIWA MANUNUZI YANALIPIWA KWA MKOPO (SIO LAZIMA)

☐ Weka alama ya vema (v) kama yamelipiwa kwa mkopo

Fomu ya mkopo

Benki inayotoa mkopo (kwa kifupi)

Jina la Tawi

## D. TAARIFA ZA MWOMBAJI

(i) Hali ya Maombi: (Weka alama ya vema panapohusika)

**Aina ya maombi:** Binafsi ☐ Kwa pamoja ☐ Taasisi ya uwekezaji yenye sifa Afrika Mashariki ☐ Taasisi ya uwekezaji yenye sifa ya Nje ☐

**Makazi:** Wakazi wa Afrika Mashariki ☐ Wasio wakaazi ☐ **Uraia:** Mtanzania ☐ Nchi nyingine za Afrika Mashariki ☐ Kimataifa ☐

(ii) **Mwombaji wa kwanza** (Taarifa za Msingi) : (Majina yaliyopo katika Kitambulisho/Pasipoti)

Jina la Kwanza na Majina Mengine (Acha nafasi kati ya jina moja na jingine)

Jina la Ukoo (Jina la Mwisho)

Namba ya Kitambulisho/ Pasipoti (Nakala ya Kitambulisho/Pasipoti lazima iambatishwe)

Nchi Ilikotolewa

(iii) **Mwombaji wa Pili** (Taarifa za Msingi) kama Pamoja: (Majina kama yalivyo katika Kitambulisho/Pasipoti)

Jina la Ukoo(Jina la Mwisho)

Jina la Kwanza na Majina Mengine(Acha nafasi kati ya jina moja na jingine)

Namba ya Kitambulisho/ Pasipoti (Nakala ya Kitambulisho/Pasipoti lazima iambatishwe)

Nchi Ilikotolewa

(iv) Jina la kampuni / QII (Kama ilivyo katika Hati ya Usajili/ Ilivyosajiliwa ) Nakala ya Hati lazima iambatishwe

Namba ya Usajili/ Kama ilivyosajiliwa

Nchi ilikosajiliwa

☐ Weka alama ya vema (v) kama maombi yamesamehewa kulipa kodi (withholding tax) na ambatanisha nakala ya hati ya msamaha.

**Kwa Waombaji Waliopendekezwa tu (Weka alama ya vema (v) panapohusika hapo chini)**

**Uraia wa Mnufaika wa Hati fungani** ☐ Mtanzania ☐ Nchi nyingine za Afrika Mashariki ☐ Nchi Nyingine za Kimataifa

Namba ya Akaunti ya Mwombaji Aliyependekezwa

Namba ya Kumbukumbu ya Mwombaji Aliyependekezwa (Lazima)

# Fomu ya maombi ya Hati fungani

Akaunti ya Malipo: **10110000587**

## (v) Anwani Kamili ya Posta na Taarifa za Mawasiliano za Waombaji Wote (kama itafaa)

S.L.P

Anwani ya Mtaa

Jiji/Mji

Nchi

Namba ya Simu (ya mezani) Mfumo wa Kimataifa

Namba ya Simu ya Mkononi Mfumo wa Kimataifa **(Lazima)**

Anwani ya Baruapepe (Binafsi)

Namba ya Faksi (Mfumo wa Kimataifa)

## E. UREJESHAJI WA FEDHA NA MALIPO YA SIKU ZA BAADAYE

1. Tuma marejesho kama yapo kupitia ☐ EFT kupitia wakala wa mauzo aliyeidhinishwa ☐ Uhamishaji wa Fedha kwa njia ya Elektroni kwenda kwenye benki iliyotajwa hapo chini
2. Tuma riba na Mtaji kupitia ☐ Uhamishaji wa Fedha kwa njia ya Elektroni kwenda kwenye benki iliyotajwa hapo chini (Kulingana na taarifa za akaunti ya CDS, kama haipo, tafadhali weka taarifa za benki zilizohuishwa hapo chini)

Tafadhali toa taarifa za benki kwa uhamishaji wa EFT/SWIFT

(Taarifa mpya za benki lazima zithibitishwe kwa kuambatanisha cheki isiyotumika au taarifa ya benki (bank statement)

Jina la Benki (kwa kifupi)

Jina la akaunti

Jina la Tawi

Namba ya akaunti

Swift Code (kama nje ya Tanzania)

Nchi

## F. SAHIHI: (LAZIMA KWA WAOMBAJI WOTE)

Sahihi ya 1

Sahihi ya 2

Mhuri wa moto / Mhuri

Tarehe (SS/MM/MMMM) mf. 27/07/2012

## G. WAKALA WA MAUZO / MATAWI YA NMB TU KWA MATUMIZI YA OFISI

Namba ya Wakala/Namba ya Tawi la NMB

Jina la Wakala wa Mauzo/Mwakilishi wa Huduma kwa Wateja wa NMB

Mhuri wa Wakala wa Mauzo Aliyeidhinishwa/ Mwakilishi wa Huduma kwa Wateja wa NMB

KATA HAPA

## H. RISITI YA MWEKEZAJI

Namba ya Kumbukumbu

Jina (Tenganisha Jina moja na Jingine kwa kuruka kiboksi kimoja)

Kiasi kilicholipwa (TShs)

Namba ya akaunti ya CDS (Isianze na sifuri)

(LI/LC/FI/FC)

Jina la Wakala wa Mauzo/ Jina la Tela wa NMB

Mhuri na sahihi ya Wakala wa Mauzo/ Tawi la NMB

Tarehe

# Fomu ya maombi ya Hati fungani

**MAELEKEZO YA KINA KUHUSU UJAZAJI WA FOMU YA MAOMBI: (Tafadhali soma maelekezo ya jumla katika ukurasa wa 1)**

A. Mwombaji lazima awe na Akaunti ya CDS ili kuomba. Kama huna akaunti ya CDS tafadhali omba kufungua akaunti hiyo kwa kujaza fomu ya kufungulia akaunti ya CDS na kuiambatisha na fomu hii ya maombi (muombe Wakala yeyote wa Mauzo Aliyeidhinishwa akusaidie). Tafadhali onyesha namba ya Fomu ya Maombi katika Fomu ya kufungulia akaunti ya CDS.

LI - Mtu binafsi - Mtanzania
LC - Kampuni ya Ndani ya Kitanzania
FI - Taasisi ya Kigeni
FC - Kampuni ya Kigeni

B. Kiwango cha chini unachoweza kuwekeza ni TZS 500,000 na baadaye kwa mafungu ya TZS 10,000 Ingiza kiwango unachopenda kuwekeza katika viboksi ulivyopewa. Kumbuka kufuata kanuni kwa kiwango cha chini cha uwekezaji na kiwango cha nyongeza pia.

- Kama Wakala wako wa Mauzo Aliyeidhinishwa anafanya malipo kwaniaba yako, tafadhali weka alama ya vema(v) ndani ya kiboksi cha malipo kupitia wakala. Huhitaji kujaza taarifa zilizobaki chini ya sehemu "B".
- Kama ungependa kufanya malipo moja kwa moja kwa mtoaji wa Hati fungani, NMB kama Wakala wako wa Mauzo Aliyeidhinishwa ataweka alama ya vema (v) katika kiboksi cha njia ya malipo inayofaa kilichoandikwa Hundi ya Benki, EFT/TISS au Barua ya Makubaliano.
- Jina la benki, tawi namba ya hundi au namba ya kumbukumbu ya EFT/TISS/ Namba ya Fomu ya Maombi lazima ionyeshwe.
- Kwa malipo ya moja kwa moja ya mtoaji, tumia taarifa zifuatazo:
  **NMB BANK TAWI LA OHIO**
  **NA. YA AKAUNTI: 10110000587**

C. Kama uwekezaji au ununuzi wako wa Hati fungani za NMB umelipiwa na benki, tafadhali kamilisha sehemu ya ulipiaji kwa kuweka alama ya vema katika kiboksi na kuingiza namba ya maombi ya mkopo, jina la benki unayokopa na jina la tawi. Fomu ya maombi ya Mkopo na siku inayotakiwa kulipwa, vitatumwa moja kwa moja kwenye DSE na benki itakayokupa mkopo.

D. TAARIFA ZA MWOMBAJI

(i) Unatakiwa kuweka alama ya vema(v) katika viboksi vitatu chini ya kichwa cha habari "Hali ya mwombaji"

- Aina ya Mwombaji: Weka alama ya vema katika kiboksi kinachohusika ambacho kinafafanua aina ya mwombaji.
- Hali ya Makazi: Kama ni MKAZI wa kudumu wa Afrika Mashariki, bila kujali uraia wako, weka alama ya vema katika kiboksi kilichoandikwa "Mkazi wa Afrika Mashariki", vinginevyo, weka alama ya vema katika kiboksi cha Asiye Mkazi
- Uraia: Weka alama ya vema katika kiboksi kinachofafanua uraia wako.

(ii) Ikiwa unaomba Hati fungani kama mtu binafsi (mf. wewe sio Kampuni ya Uwekezaji), tafadhali jaza taarifa zilizoorodheshwa chini ya maneno " Taarifa za Msingi za Mwombaji". Inapowezekana tafadhali hakikisha unaingiza namba yako ya utambulisho wa taifa (au namba nyingine za utambulisho), au namba ya pasipoti na nchi iliyotowa.

(iii) Kama unapenda kumuingiza mwenza wako au ndugu au rafiki kama maombi ya pamoja katika fomu hii, tafadhali jaza taarifa zake katika nafasi inayohusika chini ya kichwa cha habari " Taarifa za maombi ya pamoja". Tafadhali kumbuka:

- Maombi ya pamoja yanaruhusiwa MARA MOJA TU
- Maombi ya pamoja HAYAWEZI kuwa Kampuni ya Uwekezaji. Tafadhali hakikisha kuwa akaunti ya CDS ni ya pamoja pia.

Kila inapowezekana, tafadhali hakikisha unaingiza namba ya utambulisho wa maombi ya pamoja, ikishindikana, tafadhali ingiza namba yake ya Pasipoti na nchi ilikotolewa. Angalau namba MOJAWAPO ni lazima.

(iv) Iwapo unaomba kama kampuni, Taasisi yenye Sifa za Uwekezaji(QII) au mwombaji aliyeteuliwa, tafadhali jaza taarifa zote zinazotakiwa katika sehemu hii. Taarifa za sehemu hii zinaweza kupatikana katika Hati ya Usajili. Tafadhali ambatisha nakala kivuli ya Hati ya Usajili na leseni ya biashara kama Taasisi ya Uwekezaji.
Waombaji walioteuliwa kutoka katika kampuni halisi iliyosajiliwa watakubaliwa ikiwa kuna jina/namba ya pekee kwa kila maombi. Kwa ajili ya kuepuka wasiwasi, Akaunti za Walioteuliwa lazima ziwepo kwa faida ya mtu wa tatu anayehusika na maombi ya Hati fungani kulingana na haki zao. Taasisi yoyote ya Uwekezaji au Mwombaji mwenye msamaha wa kodi (withholding tax) LAZIMA AAMBATISHE NAKALA YA HATI YA MSAMAHA WA KODI.

(v) WAOMBAJI LAZIMA WAJAZE SEHEMU HII. ANWANI MOJA TU IINGIZWE.
Tafadhali ingiza ANWANI YAKO KAMILI ya posta, ikijumuisha inapofaa SLP. na Jiji/Mji na Nchi. Anwani ya Mtaa ni hiari lakini inashauriwa kutolewa ikiwa anwani ya posta itakuwepo. Anwani itatumika kwa mawasiliano yanayohusu Hati fungani, na ni muhimu kwamba taarifa zilizomo ni za kweli na sahihi, tafadhali pia tupatie namba yako ya simu ya mkononi, simu ya mezani (kama unayo) na anwani ya baruapepe.

E. RISITI KWA AJILI YA MAREJESHO:

(1) Wakazi wote watarejeshewa kwa njia ya EFT Hati fungani ambazo hazikugaiwa. Tafadhali jaza taarifa zako za benki katika viboksi ulivyopewa. Tafadhali kumbuka kwamba taarifa mpya za benki lazima zithibitishwe kwa ama kuambatisha hundii ambayo haijajazwa iliyoandikwa cancelled au taarifa ya benki ( bank statement).

(2) Marejesho yoyote yatakayolipwa kwa Mataifa ya Afrika Mashariki nje ya Tanzania (isipokuwa Taasisi yenye Sifa za uwekezaji(QII) ambayo iliwasilisha Barua za Ahadi) na Wageni

F. WAOMBAJI WOTE LAZIMA WAJAZE SEHEMU HII.

Tafadhali soma maelekezo yafuatayo kwa makini:

- Waombaji wa Awali lazima wasaini katika kiboksi kilichoandikwa “Sahihi ya 1” na Waombaji washirika (kama wapo) wasaini katika kiboksi kilichoandikwa “Sahihi 2”
- Maombi ya kampuni za uwekezaji lazima yasainiwe na watiasaini wawili wallioidhinishwa. Ikiwa mwombaji ni Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni, mhuri wa moto/mhuri wa kampunii lazima ugongwe katika nafasi iliyoachwa wazi.
- Maombi yaliyosainiwa kwa alama za vidole gumba lazima yawe na shahidi, jina lake na namba ya kitambulisho chake